

**Issue no:** 01 | **Vol no:** 06 | **September** 2025: 78-93

# Uchanganuzi wa Aina za Mandhari Kifinominolojia katika Riwaya ya *Nguu za Jadi*

**Jane Karimi Ntongai** [1]
**Rose Mavisi** [2]
**Douglas Nkumbo** [3]

**(1.2) Catholic University of Eastern Africa, Kenya; (3) Laikipia University, Kenya.**
Main author's email: jkarimin@gmail.com

**Article History**
Received: **2025.07.21**
Accepted: **2025.08.20**
Published: **2025.09.22**

**Cite this article in APA**
Ntongai, J. K., Mavisi, R., & Nkumbo, D. (2025). Uchanganuzi wa aina za mandhari kifinominolojia katika riwaya ya *Nguu za Jadi*. *Editon consortium journal of Kiswahili, 6*(1), 78-93.
https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v6i1.631

**Ikisiri**
Lengo la makala hii ni kubainisha aina za mandhari katika *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2021). Tatizo la utafiti lilitokana na ukosefu wa tafiti zilizotumia nadharia ya finominolojia kuchunguza mandhari katika fasihi ya Kiswahili. Tafiti zilizotangulia ziliangazia mandhari kama mazingira ya kijamii na kihistoria pekee, bila kuzingatia tajriba ya ndani ya wahusika kwa mtazamo wa kifinominolojia. Uchambuzi huu uliongozwa na Nadharia ya Finominolojia, iliyoasisiwa na Husserl (1970) na kuendelezwa na Heidegger (1962), Merleau-Ponty (2012) na Sartre (2003), kisha kupanuliwa na Van-Manen (2017) na Zahavi (2019). Finominolojia ni mwelekeo wa kifalsafa unaozingatia namna binadamu wanavyoishi na kupokea tajriba zao bila upendeleo wa awali. Utafiti ulitumia muundo wa kimaelezo, ambapo *Nguu za Jadi* iliteuliwa kimaksudi kwa upekee wake katika kusawiri changamoto za kijamii. Data zilikusanywa kupitia usomaji wa kina na kudondoa hoja muhimu zinazohusiana na malengo ya utafiti. Matokeo yalibainisha kuwa mandhari katika *Nguu za Jadi* yanajitokeza kwa aina tatu kuu: mandhari ya kimahali, mandhari ya kiwakati na mandhari ya kihali. Mandhari haya huchangia katika kujenga wahusika na kufanikisha uwasilishaji wa ujumbe wa kijamii, kisiasa na kitamaduni. Kwa jumla, utafiti huu umeonyesha nafasi ya mandhari katika kuakisi maisha ya Kiafrika na kusisitiza umuhimu wa mtazamo wa kifinominolojia katika fasihi. Matokeo yake yanatoa mwongozo wa kitaaluma kwa waandishi, watafiti na wabunifu wa mitaala.

**Maneno muhimu**: Finominolojia, mandhari, mgogoro, riwaya, uzoefu.

Editon OPEN ACCESS

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

## UTANGULIZI

Mandhari ni kipengele muhimu katika fasihi kwa kuwa huwasilisha hali za kijamii, kitamaduni, kisiasa, kiuchumi na kihisia. Hata hivyo, tafiti nyingi za fasihi ya Kiswahili zimezidi kulichukulia mandhari kama mazingira ya nje pekee, bila kuangazia nafasi yake katika kujenga wahusika na kufikisha ujumbe wa fasihi. Pengo hili limechangiwa pia na ukosefu wa tafiti zinazotumia mtazamo wa kifinominolojia kueleza jinsi wahusika wenyewe wanavyopokea na kuishi mandhari katika tajriba zao za kila siku.

Mapengo makuu ya kitaaluma yanayojitokeza ni matatu. Kwanza, hakuna tafiti nyingi zilizotumia nadharia ya kifinominolojia kuchambua mandhari katika fasihi ya Kiswahili. Pili, uhusiano wa moja kwa moja kati ya mandhari na ujenzi wa sifa za wahusika haujaelezwa kwa kina. Tatu, tafiti zilizopo hazijatoa msisitizo wa kutosha kwa ujumbe wa kijamii, kitamaduni na kisiasa unaoibuliwa na mandhari. Utafiti huu unakusudia kuziba mapengo haya kwa kuchunguza mandhari katika riwaya ya *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2021) kwa mtazamo wa kifinominolojia, ili kuonyesha namna yanavyojenga wahusika, kusababisha migogoro na kuibua ujumbe wa fasihi.

Kwa mujibu wa watafiti kama Kilonzo (2020), mandhari ya kijamii na kitamaduni yanaweza kufafanua tabia za wahusika kwa undani, ilhali Makori (2019) anaona mtazamo wa kifinominolojia kama nyenzo ya kuelewa uhusiano kati ya wahusika na mazingira yao. Kadhalika, Kamara (2021) anaonyesha kwamba mandhari yanaweza kuakisi mabadiliko ya kijinsia na kijamii, huku Komba (2019) akikiri kuwa tafiti za aina hii katika fasihi ya Kiswahili bado hazijapewa kipaumbele. Hata hivyo, hakuna kati ya tafiti hizi zilizojikita mahsusi katika riwaya ya *Nguu za Jadi*, jambo linalothibitisha haja ya utafiti huu.

Katika makala hii, istilahi kuu zinazoongoza mjadala ni: finominolojia, inayomaanisha mwelekeo wa kifalsafa unaochunguza tajriba hai za binadamu; mandhari, yanayohusu mazingira ya kimahali, kiwakati na kihali; migogoro, ikimaanisha mvutano na mabadiliko yanayoathiri wahusika; riwaya, kama utanzu wa simulizi refu; na uzoefu, unaojumuisha hali na matukio yanayowakumba wahusika katika maisha ya kijamii na kitamaduni.

Kwa jumla, makala hii itachunguza aina za mandhari katika *Nguu za Jadi* na kuonyesha mchango wake katika kuunda wahusika na migogoro pamoja na kufikisha ujumbe wa kijamii, kisiasa na kitamaduni. Upekee wa riwaya hii katika kusawiri changamoto za uongozi, ukosefu wa maadili, dhuluma za kijinsia na mshikamano wa kifamilia ndio unaoiweka kama chaguo mwafaka la kuchunguza nafasi ya mandhari kupitia mtazamo wa kifinominolojia.

## MAPITIO YA MAANDISHI

### Dhana ya Riwaya na Muktadha wa *Nguu za Jadi*

Riwaya ni utanzu wa fasihi andishi wenye upeo mpana wa simulizi, ikijengwa kwa visa virefu vinavyowahusu wahusika mbalimbali katika mazingira tofauti ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kihisia. Kwa mujibu wa Khamis (2020), riwaya ya Kiswahili katika karne ya ishirini na moja imekuwa nyenzo mahususi ya kuchunguza masuala ya ukandamizaji, ukosefu wa haki na changamoto za kijamii zinazojitokeza katika maisha ya kila siku. Aidha, Diegner (2021) anaeleza kuwa riwaya za Kiswahili za sasa zinatumia mbinu za kifasihi zinazozingatia upeo wa kijamii na kihisia kwa lengo la kuibua sauti za waliotengwa na kuhoji mifumo kandamizi ya kiutawala. Vilevile, Ngure (2019) anasisitiza kwamba riwaya hufanya kazi kama ukosoaji wa kijamii unaolenga kusawiri maisha ya binadamu katika uhalisia wake na kuibua mwelekeo wa mabadiliko ya kijamii na kisiasa.

Riwaya ya *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2021) ni miongoni mwa maandiko mapya katika fasihi ya Kiswahili yanayoshughulikia changamoto za kijamii, kisiasa na kimaadili katika taifa la kifasihi la Matuo. Dhima kuu ya riwaya hii ni ukosoaji wa mifumo dhalimu ya uongozi, ukosefu wa maadili, dhuluma za kijinsia na kuporomoka kwa mshikamano wa kifamilia. Kupitia wahusika kama Mangwasha, Mrima, na Sagilu, riwaya inafichua namna tamaa, ufisadi na mfumo dume vinavyoathiri maisha ya watu wa kawaida, huku ikiibua taswira ya matumaini na ukombozi wa kijamii kupitia viongozi wapya wenye dhamira ya kweli ya mabadiliko.

Katika muktadha wa fasihi ya Kiswahili, *Nguu za Jadi* inachukua nafasi muhimu kwa kutumia mtazamo wa kifinominolojia kuonyesha mandhari kama tajriba hai ya kifamilia, kijamii na kisiasa. Riwaya hii inaendeleza mjadala wa fasihi za kijamii na kihistoria kwa kuunganisha uhalisia wa maisha na sauti ya ukombozi, hivyo kuijengea hadhi kama maandiko ya kisasa

yanayopanua upeo wa fasihi ya Kiswahili katika karne ya 21.

**Mandhari katika Fasihi**

Mandhari yamejadiliwa na wataalamu kwa mitazamo tofauti. Wamitila (2002, 2003, 2008) anayaeleza kama sehemu ya matukio ya kifasihi, akionyesha mchango wake katika kufafanua wahusika na maudhui. Hata hivyo, mtazamo wake unabaki katika kipengele cha fani bila kuangazia namna mandhari huishiwa na wahusika. Vilevile, Njogu na Chimera (2008) wanapanua maana ya mandhari kwa kuyahusisha na nyanja za kijamii, kiutamaduni na kihistoria, lakini mchango wao unabaki wa kijumla na haueleza tajriba ya ndani ya mhusika. Utafiti huu unajitofautisha kwa kuchunguza riwaya ya *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2021) kwa mtazamo wa kifinominolojia, ambapo mandhari yanaangaliwa kama tajriba hai inayoumba na kuundwa na hisia pamoja na mitazamo ya wahusika.

Aidha, Ntarangwi (2004) katika *Uhakiki wa kazi za fasihi* anasisitiza kuwa mandhari ni msingi wa kuelewa kazi yoyote ya fasihi kwa kuwa huchota maudhui kutoka katika mazingira na historia ya mwandishi. Mtazamo huu unaonyesha uhusiano wa karibu kati ya fasihi na muktadha wa kijamii na kihistoria, na hivyo unarutubisha utafiti huu kwa kusisitiza kwamba mandhari hayawezi kutenganishwa na mazingira yanayozalisha kazi ya fasihi. Hata hivyo, hoja za Ntarangwi hazitoi msisitizo wa namna mandhari hayo yanavyopokelewa na kuishiwa na wahusika kwa mtazamo wa kifinominolojia. Utafiti wa sasa unaziba pengo hilo kwa kuchunguza riwaya ya *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2021), ambapo mandhari yanaangaliwa kama tajriba hai inayoundwa na hisia, mitazamo na hali halisi ya wahusika, badala ya kubaki katika uhalisia wa kijamii na kihistoria pekee.

Katika nadharia ya kifalsafa, Bachelard (1994) anatazama mandhari kama nafasi inayojengwa na fikra na hisia, ambapo wahusika huishi ndoto na kumbukumbu zao. Mtazamo huu unaonyesha kwamba mandhari yana sura ya kiakili na kihisia ambayo huathiri namna wahusika wanavyotambua ulimwengu wao. Kadhalika, Cresswell (2015) anaeleza mandhari kama uzoefu unaobeba historia, mitazamo na hisia za binadamu, akisisitiza mwingiliano kati ya mtu na mazingira. Pamoja na umuhimu wake, Bachelard hakuielekeza dhana hii katika uchambuzi wa fasihi ya Kiswahili, na Cresswell naye hakujikita moja kwa moja katika muktadha wa kazi za kifasihi. Utafiti wa sasa, kwa kuchunguza riwaya ya *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2021), unaziba pengo hilo kwa kusisitiza mandhari kama sehemu ya tajriba ya moja kwa moja ya wahusika inayoundwa na maisha yao ya kijamii, kihisia na kifikra.

Katika fasihi ya Kiswahili, Bahati (2014) alichunguza tamthilia ya *Mashetani* ya Ebrahim Hussein na kubainisha kuwa mandhari ya kijamii na kihistoria huchangia kuibua maudhui ya ukoloni, ukoloni mamboleo na migongano ya kitabaka. Ingawa mchango huu ni wa msingi katika kueleza nafasi ya mandhari, utafiti huo ulijikita zaidi katika utanzu wa tamthilia na katika uhusiano wa moja kwa moja kati ya mandhari na maudhui, bila kuangazia mandhari kama tajriba ya ndani inayopokelewa na kuishiwa na wahusika. Kwa hivyo, utafiti wa Bahati una umuhimu mkubwa kwa utafiti huu kwa kuwa ulitoa mwanga kuhusu jinsi mandhari yanavyoweza kufanikisha uwasilishaji wa maudhui. Hata hivyo, utafiti huu unajitofautisha kwa kulenga utanzu wa riwaya na kuangazia mandhari kupitia mtazamo wa kifinominolojia, ambapo uzoefu wa ndani wa wahusika katika kuishi na kutafsiri mandhari ndio kiini cha uchambuzi.

Vivyo hivyo, Muia (2023) walihakiki riwaya ya *Maisha Kitendawili* ya John Habwe na kubainisha kuwa mandhari ni uti wa mgongo wa uwasilishaji wa ujumbe wa mwandishi. Walionyesha jinsi mandhari ya tabaka la juu na la chini, chuo na kanisa yalivyotumika kusawiri maadili na changamoto za kijamii kwa kutumia nadharia ya uhalisia. Mfanano wa msingi kati ya utafiti wao na huu ni kwamba wote wanatambua nafasi ya mandhari kama nyenzo kuu katika ujenzi wa ujumbe wa fasihi ndani ya riwaya. Hata hivyo, tofauti kuu ipo katika nadharia zilizotumika. Utafiti wa Muia na wenzake ulijikita katika nadharia ya uhalisia, ukisisitiza taswira za kijamii na kitabaka, ilhali utafiti huu unatumia nadharia ya kifinominolojia kwa kusisitiza namna wahusika wanavyopokea na kuishi mandhari hayo kama tajriba ya ndani. Kwa hivyo, utafiti wa sasa unajitokeza kwa kuangazia upeo mpya wa uelewa wa mandhari kwa kuhusisha moja kwa moja maisha ya ndani ya wahusika na uzoefu wao wa kijamii na kihisia.

Kutokana na mapitio haya, ni dhahiri kwamba tafiti nyingi zimeeleza mandhari kama kipengele cha fani na uhalisia wa kijamii. Pengo linalobaki ni ukosefu wa tafiti zinazochunguza mandhari kama uzoefu hai wa kifinominolojia, yaani namna wahusika wanavyopokea, kuishi na kuunda maana kupitia mandhari. Utafiti huu wa

riwaya ya *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2021) unalenga kuziba pengo hilo. Kupitia mihimili ya kifinominolojia, ulichunguza namna mandhari ya kimahali, kiwakati na kihali yanavyopokelewa na kuishiwa na wahusika, ili kuthibitisha kuwa mandhari si taswira ya kijiografia pekee, bali ni uzoefu unaojenga uhusiano kati ya binadamu na ulimwengu wao.

**Mandhari ya Kimahali**

Mandhari ya kimahali yanahusu maeneo ya kijiografia na kimaeneo ambamo wahusika huishi na kutenda. Cresswell (2015) anabainisha kuwa nafasi si eneo la kijiografia pekee, bali ni tajriba inayoundwa na watu wanaoishi ndani yake. Hoja hii ni muhimu kwa utafiti huu kwa sababu inasisitiza mandhari kama uzoefu hai wa binadamu. Hata hivyo, mchango wa Cresswell umejikita zaidi katika mifumo ya kijamii na kijiografia ya Magharibi na haujaangazia fasihi ya Kiswahili. Pengo hili ndilo utafiti wa sasa unaliziba kwa kuchunguza riwaya ya *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2021) kupitia mtazamo wa kifinominolojia, ili kubainisha namna mandhari ya kimahali yanavyopokelewa, kuishiwa na kuathiri maisha ya ndani ya wahusika katika muktadha wa kijamii na kitamaduni wa Kiafrika. Tofauti na mtazamo wa Cresswell unaobaki katika upeo wa kijamii wa Magharibi, utafiti huu unapanua wigo huo kwa kuuangazia ndani ya fasihi ya Kiswahili na kwa kuhusisha tajriba ya moja kwa moja ya wahusika.

Mjadala kuhusu mandhari ya kimahali umeendelezwa na wataalamu mbalimbali. Tally (2013) anaunganisha mandhari na masimulizi ya kijiografia katika fasihi ya dunia na kuonyesha kuwa nafasi hubeba simulizi na maana za kijamii. Bal (2017) anasisitiza athari za mandhari katika mienendo ya wahusika na mtazamo wa wasomaji, huku Miller (2020) akibainisha uwezo wa mandhari kubadilisha muundo wa simulizi. Mawazo haya yana umuhimu mkubwa kwa utafiti wa sasa kwa kuwa yanaeleza jinsi vijiji kama Ndengoni na Munyuni pamoja na mijini kama Taria, Matango, Majengo na Majuu katika *Nguu za Jadi* yanavyounda uhusiano wa kijamii, kuathiri mienendo ya wahusika na kuongoza mwendelezo wa matukio.

Pamoja na mchango wao, tafsiri za Tally, Bal na Miller zimejikita zaidi katika fasihi ya kigeni na zimesalia katika upeo wa kijumla, bila kuonyesha kwa undani namna wahusika wanavyopokea mandhari na kuyafanya kuwa sehemu ya tajriba yao ya ndani katika muktadha wa Kiafrika. Utafiti huu unatofautiana nao kwa kuangalia mandhari ya kimahali katika *Nguu za Jadi* kupitia mtazamo wa kifinominolojia, ambapo nafasi hazionekani tu kama alama za kijamii na kijiografia, bali kama mazingira yanayoishi katika fahamu na hisia za wahusika.

Katika muktadha wa Kiafrika, Wanjala (2018) kupitia kazi yake *Mandhari katika fasihi ya Kiswahili* anaonyesha ukinzani kati ya mila na kisasa unaojitokeza kupitia mandhari ya vijijini. Mtazamo huu unaendana na riwaya ya *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2021), ambapo mandhari ya vijijini na mijini yanabeba mapambano kati ya maadili ya jadi na mabadiliko mapya ya kijamii. Ingawa mchango wa Wanjala ni muhimu katika kufafanua maana ya mandhari kwa ngazi ya kijamii na kitamaduni, utafiti wake haukuzingatia namna wahusika wanavyopokea na kuishi mandhari hayo katika kiwango cha kisaikolojia na kihisia. Utafiti wa sasa unaliziba pengo hili kwa kutumia mtazamo wa kifinominolojia ili kuonyesha mandhari kama tajriba ya ndani ya wahusika.

Naye, Cosmas (2021) katika *Usawiri wa Mandhari katika riwaya* alitumia nadharia ya kifinominolojia kuchunguza riwaya za watoto kama *Embe Tamu* (Njogu, 2003), *Siku ya Wajinga* (Momanyi, 2005) na *Njiapanda* (Amana, 2008). Alibainisha mandhari ya nyumbani, shuleni, sokoni na hospitalini, yaliyowasilisha maudhui ya elimu, urafiki, teknolojia na biashara. Mchango huu unaonyesha jinsi mandhari yanavyosaidia kufanikisha dhamira katika fasihi ya watoto.

Hata hivyo, utafiti wake ulijikita zaidi katika kuainisha aina za mandhari na haukuchunguza namna wahusika wanavyoyaishi au kuyapokea kisaikolojia. Aidha, ulihusu fasihi ya watoto pekee. Utafiti wa sasa unajitofautisha kwa kuchunguza *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2021) katika fasihi ya watu wazima, ambapo mandhari ya kimahali yanaelezwa kama tajriba hai inayoshirikiana na hisia na mitazamo ya wahusika, hivyo kuziba pengo lililoachwa na utafiti wa Cosmas.

Kwa jumla, mapitio ya maandishi yanaonesha kuwa wataalamu kama Cresswell (2015), Tally (2013), Bal (2017), Miller (2020) na Wanjala (2018) wameeleza umuhimu wa mandhari ya kimahali katika kufafanua uhusiano wa kijamii, kitamaduni na kimaudhui katika fasihi. Hata hivyo, mitazamo yao imeegemea zaidi fasihi ya kigeni au imebaki katika ngazi ya kijumla bila kuchunguza tajriba ya ndani ya wahusika. Vilevile, Cosmas (2021) alitumia nadharia ya kifinominolojia

kuchunguza mandhari katika fasihi ya watoto, akisisitiza aina na kazi zake lakini bila kufafanua kwa kina namna wahusika wanavyoyaishi kisaikolojia na kihisia.

Utafiti wa sasa unajitofautisha kwa kuchunguza riwaya ya *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2021) katika muktadha wa fasihi ya watu wazima, ambapo mandhari ya kimahali hayachukuliwi tu kama mazingira ya kijamii bali kama tajriba hai inayoshirikiana na hisia na mitazamo ya wahusika, hivyo kuziba pengo lililoachwa na tafiti zilizotangulia.

**Mandhari ya Kiwakati**
Mandhari ya kiwakati hurejelea muda, historia na muktadha wa kijamii unaojitokeza katika kazi za fasihi. Katika *Time and Narrative*, Ricoeur (1984) anaeleza kuwa simulizi hupata maana kupitia muda, akibainisha kwamba muda huunda muktadha wa matukio na namna wahusika wanavyouishi. White (2014), katika *The Practical Past*, anapanua hoja hii kwa kuonyesha kuwa historia katika fasihi ni chombo cha kueleza siasa, itikadi na mitazamo ya kijamii. Michango yao inafafanua nafasi ya wakati katika uundaji wa maana, lakini haielezi namna wahusika huishi na kutafsiri muda huo katika kiwango cha kisaikolojia na kihisia.

Bal (2017), kupitia *Narratology*, anaonyesha kuwa muda huathiri mienendo ya wahusika na mtazamo wa wasomaji, huku Tally (2013) katika *Spatiality* akihusisha muda na ramani za kijamii na kisiasa. Aidha, Eagleton (2012) anabainisha fasihi kama kioo cha historia ya kijamii. Hata hivyo, tafiti hizi zimejikita zaidi katika fasihi ya kigeni na mitazamo ya kifalsafa bila kuangazia uzoefu wa ndani wa wahusika.

Katika muktadha wa Kiswahili, Cosmas (2021) alichunguza historia kama chombo cha kufafanua migogoro ya kijamii katika hadithi fupi, huku Okoth (2017) akihusisha mabadiliko ya kijinsia na vipindi vya kihistoria. Wanjala (2018), katika *Mandhari katika Fasihi ya Kiswahili*, alionyesha athari za historia ya ukoloni na uhuru katika kuibua migongano ya kitamaduni. Tafiti hizi zinaonyesha mchango muhimu katika kueleza nafasi ya historia na muda katika fasihi ya Kiswahili, lakini zimejikita zaidi katika hadithi fupi na tamthilia, na hazijaonyesha namna wahusika binafsi wanavyopokea na kuishi mandhari ya kiwakati.

Mavisi (2022), katika makala yake *Usawiri wa mandhari kibibliotherapia katika hadithi fupi teule za kiswahili*, alibainisha mandhari ya asubuhi na usiku kama vipengele vya muda vinavyochochea hisia na mitazamo ya wahusika. Asubuhi iliashiria matumaini na mwanzo mpya, ilhali usiku ulihusishwa na hofu na huzuni. Mchango huu ni muhimu kwa utafiti wa sasa kwa kuwa unaonyesha muda kama chanzo cha maana ya kihisia katika fasihi. Hata hivyo, utafiti wa Mavisi ulihusu hadithi fupi na ukiongozwa na Nadharia ya Mapatano ya Mwitikio wa Msomaji, hivyo haukuzingatia tajriba ya kifinominolojia ya wahusika. Utafiti huu, unaolenga riwaya ya *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2021) kwa kutumia Nadharia ya Finominolojia, unaziba pengo hilo kwa kuonyesha mandhari ya kiwakati kama uzoefu hai wa kihisia na kisaikolojia wa wahusika.

Kwa msingi huu, utafiti wa sasa unajitofautisha kwa kuchunguza riwaya ya *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2021) kwa mtazamo wa kifinominolojia. Riwaya hii inaonyesha jinsi mandhari ya mchana, usiku na mabadiliko ya kihistoria yanavyopokelewa na kuishiwa na wahusika kama sehemu ya hisia na maamuzi yao. Hivyo, utafiti huu unaziba pengo kwa kuangalia mandhari ya kiwakati kama tajriba ya ndani inayounda maana ya maisha ya wahusika katika muktadha wa Kiafrika.

**Mandhari ya Kihali**
Mandhari ya kihali yamekuwa yakihusishwa na hisia, mitazamo na hali ya kisaikolojia ya wahusika. Bachelard (1994), kupitia *The Poetics of Space*, anabainisha kuwa nafasi ni hifadhi ya kumbukumbu na hisia binafsi zinazounda tajriba ya ndani ya mhusika. Mtazamo huu unasaidia utafiti wa sasa kwa kusisitiza kuwa mandhari si tu alama za kijiografia, bali ni sehemu hai ya maisha ya ndani ya binadamu. Hata hivyo, mchango wa Bachelard unajikita zaidi katika falsafa ya Magharibi na haujaangazia fasihi ya Kiafrika, jambo linalofanya utafiti huu kuupanua mtazamo huo kwa kuutumia katika uchambuzi wa *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2021).

Aidha, Fennell (2017) na Garcia (2018) walionyesha kuwa mandhari hubadilika kulingana na hisia za mhusika, ambapo mazingira ya huzuni au furaha huakisi maisha ya ndani ya mtu. Mchango huu ni msingi wa kuelewa mandhari ya huzuni na mateso katika *Nguu za Jadi*, hasa kupitia wahusika kama Mangwasha na Lonare. Tofauti ni kwamba tafiti zao zilibaki katika upeo wa fasihi ya kimataifa na hazikujikita kwenye riwaya za Kiswahili.

Kwa upande wa kifalsafa, Zahavi (2019) alisisitiza kuwa hisia ndizo njia ya mtu kuishi ulimwengu, na Van Manen (2017) akabainisha mandhari kama uzoefu wa kiutendaji unaoathiri nafsi na mwili. Mchango huu unaimarisha msingi wa kifinominolojia wa utafiti wa sasa, ingawa tafiti hizi hazikuonyesha wazi namna mandhari yanavyoshirikiana na maisha ya kijamii ya Kiafrika.

Katika fasihi ya Kiswahili, Kyalo (2021) alihusisha mandhari ya kihali katika hadithi fupi na hisia za huzuni, hofu na furaha; Wanjala (2018) akaonyesha mivutano ya kifamilia na kitamaduni kupitia mandhari hayo, huku Mbaria (2016) akieleza mandhari kama kioo cha kukata tamaa kulikozushwa na ukoloni. Hata hivyo, tafiti hizi ziliishia zaidi kwenye tanzu fupi kama hadithi na ushairi na hazikuzingatia riwaya za Kiswahili, pengo linalofanyiwa kazi na utafiti huu.

Vilevile, Bahati (2014) katika uhakiki wa *Mashetani* alihusisha mandhari ya kihali na hisia za ukandamizaji, lakini hakulenga tajriba ya kifinominolojia ya wahusika. Kwa upande mwingine, Muia et al. (2023) walichunguza riwaya ya *Maisha Kitendawili* na kuonyesha mandhari ya kihali katika chuo, nyumbani na kanisani, yakidhihirisha tofauti za kitabaka na migongano ya maadili. Ingawa utafiti wao una mchango mkubwa, uliongozwa na nadharia ya uhalisia na ulisisitiza zaidi ujumbe wa kijamii kuliko tajriba ya ndani ya wahusika.

Kwa kuzingatia mapungufu haya, utafiti wa sasa unajitofautisha kwa kuchunguza *Nguu za Jadi*, riwaya ya kisasa inayoshughulikia masuala ibuka kama ukabila, mizozo ya kifamilia na mapambano ya madaraka. Katika riwaya hii, mandhari ya kihali yanaibuka si kama alama za huzuni au furaha pekee, bali kama tajriba hai inayoundwa na hisia, mitazamo na maamuzi ya wahusika. Kwa njia hii, utafiti huu unaziba pengo lililoachwa na tafiti zilizotangulia kwa kusisitiza mandhari ya kihali kama uzoefu wa kifinominolojia unaoishiwa na wahusika moja kwa moja.

## Msingi wa Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Kifinominolojia, mwelekeo wa kifalsafa unaochunguza namna watu hupokea, kuishi na kupata uzoefu wa hali halisi kutoka mtazamo wa ndani. Smith na Osborn (2020) wanaeleza kuwa kifinominolojia huzingatia jinsi mambo yanavyodhihirika kwa anayeyapitia, badala ya kuyapima kwa mitazamo ya nje. Katika utafiti huu wa *Nguu za Jadi* ya Clara Momanyi, nadharia hii ni msingi wa kuelewa jinsi mandhari yanavyoakisiwa na kuathiri maisha ya wahusika.

Asili yake inatokana na kazi za (Husserl, 1970/1900) aliyeanzisha dhana ya *epoche* na kiini cha uzoefu. Martin Heidegger aliendeleza dhana ya *being-in-the-world* (1962), akisisitiza kutotenganishwa kwa binadamu na mazingira. Merleau-Ponty (1945/2012) aliongeza mtazamo wa *umwili* (embodiment), huku Sartre (1943/2003) akiunganisha kifinominolojia na falsafa ya uwepo kwa kusisitiza uhuru wa kuchagua na kutenda.

Wataalamu wa kisasa wamepanua misingi hii: Van Manen (2017) alisisitiza *lived experience* kama msingi wa maana ya maisha; Zahavi (2019) alieleza nafasi ya *Intentionality*; Finlay (2014) aliongeza dhana ya *Reflexivity* kuhusu nafasi ya mtafiti; na **Giorgi** (2009) alitengeneza mbinu mahsusi za matumizi yake katika sayansi ya kijamii. Michango hii inaonyesha kuwa kifinominolojia huchukulia mandhari si mazingira ya nje pekee, bali tajiriba hai inayounda uhusiano wa ndani kati ya wahusika na ulimwengu wao.

## Mihimili ya Kifinominolojia

Miongoni mwa mihimili kumi ya nadharia hii, utafiti huu ulichagua mihimili sita mahsusi kama dira ya kutimiza malengo ya kiutafiti:

Kiini cha Uzoefu – kubaini sifa kuu zinazounda mandhari katika *Nguu za Jadi*, ikiwemo vipengele vya kijamii, kisiasa na kitamaduni.
Uhalisi wa Mambo – kuchunguza mandhari jinsi yanavyojitokeza kwa wahusika bila mtazamo wa nje.
Uzoefu Halisi – kufuatilia namna wahusika huathiriwa kimwili, kihisia na kimaamuzi na mazingira yao.
Umakini wa Fahamu – kuonyesha jinsi mandhari yanavyoelekeza au kuchochea fikra na maamuzi ya wahusika.
Usisitizaji wa Maana – kueleza namna mandhari yanavyounda maana kwa wahusika na wasomaji.
Uhalisia wa Kihistoria na Kitamaduni – kubainisha jinsi mandhari yanavyoakisi historia, urithi na maadili ya jamii.

Kwa hivyo, kila lengo la utafiti huu lilitimizwa kwa kutumia mihimili miwili ya kifinominolojia. Lengo la kwanza la kubainisha aina za mandhari lilifanikishwa kwa kuhusisha kiini cha uzoefu, na uhalisia wa mambo jinsi yanavyojitokeza.

**MBINU ZA UTAFITI**

Muundo wa utafiti huu ni wa kimaelezo na uliokusudia kuchunguza kwa kina maana na uzoefu wa mandhari katika matini za kifasihi. Braun na Clarke (2021) wanaeleza kuwa uchambuzi wa kimaelezo hulenga kufichua mifumo ya maana kwa kutumia tathmini ya kina ya yaliyomo kwa kuzingatia muktadha wa kijamii na kiutamaduni. Hali hii inahusiana moja kwa moja na lengo la utafiti huu, ambalo ni kuchunguza mandhari katika riwaya ya *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2021) kwa kutumia mihimili ya Nadharia ya Kifinominolojia. Aidha, Flick (2022) anabainisha kuwa mbinu za kimaelezo hufaa zaidi pale ambapo utafiti unakusudia kuelewa jinsi fasihi inavyoweza kuakisi uzoefu wa kibinadamu kwa mtazamo wa ndani.

Utafiti huu ulijikita katika fasihi andishi, hususan utanzu wa riwaya, ambao ni mojawapo ya tanzu kuu za fasihi. Riwaya ya *Nguu za Jadi* iliteuliwa kimaksudi kwa sababu inashughulikia changamoto ibuka za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kitamaduni kama vile ukabila, ufisadi, uongozi na mapambano ya kijinsia. Kwa mujibu wa Palinkas et al. (2015), uteuzi wa kimaksudi hutoa nafasi ya kuchunguza kwa undani vipengele vinavyohusiana moja kwa moja na malengo ya utafiti. Hivyo basi, riwaya hii ilibeba upekee wa kutosheleza shabaha ya kifinominolojia ya utafiti huu.

Utafiti huu ulitumia mbinu ya ukusanyaji data ya kimaandishi kupitia usomaji wa kina wa riwaya na mapitio ya vyanzo husishi vya kifasihi na kifalsafa. Taarifa zilikusanywa kutoka maktaba ya Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki pamoja na hifadhidata za kitaaluma za mtandaoni, zikiwemo Google Scholar na JSTOR, ambazo ziliruhusu upatikanaji wa marejeleo thabiti na yanayokidhi malengo ya utafiti. Vilevile, maandiko ya kifalsafa ya waanzilishi wa kifinominolojia kama Husserl (1970/1900), Heidegger (1962), Merleau-Ponty (2012/1945) na Sartre (2003/1943), pamoja na mawazo ya wataalamu wa karibuni kama Giorgi (2009), Van Manen (2017) na Zahavi (2019), yalitumiwa kama msingi wa kinadharia katika uchambuzi wa data.

Uchanganuzi wa data ulifanywa kwa mujibu wa kanuni za kifinominolojia. Hatua ya kwanza ilihusisha usomaji wa jumla wa riwaya ili kujenga taswira ya awali ya kazi, ikifuatiwa na hatua ya epoche ambapo mtafiti aliweka pembeni mitazamo ya awali na upendeleo binafsi ili kuruhusu matini yenyewe kujidhihirisha. Baada ya hapo, mandhari yalitambulishwa na kuainishwa kwa mujibu wa vipengele vya kimahali, kiwakati na kihali, na kisha yakachunguzwa kwa kuhusiana na wahusika, hasa namna mazingira hayo yalivyoathiri hisia, mitazamo na maamuzi yao. Uchanganuzi uliendelea kwa kulinganisha maana za mandhari katika muktadha wa kijamii, kisiasa na kitamaduni, ili kufafanua athari zake kwa jamii kwa upana zaidi. Hatua ya mwisho ya uchambuzi ilikuwa ni kufikia kiini cha uzoefu wa kifinominolojia, yaani kubaini maana kuu ya mandhari katika riwaya hii.

Uwiano kati ya nadharia na mbinu ulijitokeza wazi katika mchakato wa utafiti huu. Mihimili ya kifinominolojia ndiyo iliyoongoza hatua zote za uchambuzi. *Epoche* pamoja na dhana ya kiini cha uzoefu zilitumika mwanzoni mwa uchambuzi ili kuhakikisha mandhari yalichunguzwa kwa mtazamo huru na wa moja kwa moja. Dhima ya *Intentionality* na *Lived experience* ilisaidia kufafanua jinsi wahusika walivyoyapokea mandhari na jinsi walivyoyaishi kama sehemu ya maisha yao ya ndani. Aidha, usisitizaji wa maana na kuzingatia uhalisia wa kihistoria na kitamaduni uliongoza tafsiri ya ujumbe mpana wa kijamii, kisiasa na kiutamaduni ulioibuliwa na mandhari. Hivyo basi, kulikuwa na mshikamano kati ya nadharia na mbinu, ambapo kila mhimili uliongoza hatua mahsusi za uchambuzi na kuhakikisha kuwa matokeo yanayoibuka yalikuwa na uthabiti wa kisayansi na uhalali wa kifalsafa.

Masuala ya kimaadili pia yalizingatiwa kwa umakini. Data zilizokusanywa zilihifadhiwa kwa usalama na zilitumika pekee kwa minajili ya utafiti huu, ili kulinda usiri na uadilifu wa taarifa. Hatua za kuepuka wizi wa kitaaluma zilizingatiwa kwa kutambua na kunukuu vyanzo vyote kwa mujibu wa mfumo wa APA Toleo la Saba. Aidha, barua za idhini kutoka Chuo Kikuu cha Kikatoliki cha Afrika Mashariki na NACOSTI zilipatikana kabla ya kuanza kwa utafiti, jambo lililodumisha heshima na uhalali wa kitaaluma wa mchakato mzima.

**MATOKEO YA UTAFITI**

Utafiti huu ulilenga kubainisha mandhari mbalimbali katika riwaya ya *Nguu za Jadi* ili kufanikisha shabaha la kwanza la utafiti. Mwandishi hujenga mandhari ya kijamii, kisiasa, kiutamaduni, kijinsia, kiwakati na kijiografia ili kuibua hali halisi ya maisha na migogoro ya wahusika. Uchambuzi ulizingatia mihimili miwili ya Nadharia ya Kifinominolojia: kiini cha uzoefu, kilichosaidia kutambua sifa kuu za aina mbalimbali za mandhari, na uhalisia wa mambo, uliobainisha namna

mandhari yanavyodhihirika bila upendeleo. Kupitia misingi hii, maana halisi ya mandhari katika muktadha wa fasihi ilifafanuliwa.

**Mandhari ya Mahali**

Katika *Nguu za Jadi*, mandhari ya mahali yanaibuka kama muktadha hai unaounganisha mazingira na tajriba za kihisia, kijamii na kisaikolojia za wahusika. Hali hii inapanua hoja za Kyalo (2021) kwa mtazamo wa kifinominolojia unaoonyesha mandhari kama tajriba hai badala ya kuwa mandhari ya matukio pekee. Kwa kutumia dhana ya kiini cha uzoefu, mandhari yanaonyesha hisia na athari za matukio kwa wahusika, ilhali uhalisia wa mambo unaibua changamoto za kijamii, kisiasa na kiuchumi katika jamii ya Matuo.

**Nchi ya Matuo**

Mandhari ya Matuo yanaakisi mfumo dhalimu wa kijamii na kisiasa unaojengwa juu ya ukandamizaji, ubaguzi na uharibifu wa mazingira, huku wananchi wa kawaida wakisukumwa pembezoni na viongozi na matajiri wakinufaika. Katika kuelezea hali ya maisha ya wananchi wa Matuo, msimulizi anasema:

> *Katika nchi ya Matuo, wananchi wengi pia walifukarishwa na sera za ubaguzi. Nchi ilishikia utabaka, matajiri wakawa ndio wenye nchi na wananchi wakasalia kuwa wana wa nchi.* (uk. 45)

Matini hii inaibua kiini cha uzoefu cha hali ya kukata tamaa kwa wananchi wa kawaida. Kwa kutumia lugha ya kifasihi, msimulizi anaweka wazi tofauti ya kitabaka kwa kutumia taswira ya *"wenye nchi"* dhidi ya *"wana wa nchi"*. Hali hii inamaanisha kuwa haki ya uraia imeporwa na kuwekewa vigezo vya mali na nafasi ya kijamii. Kwa mtazamo wa kifinominolojia, msomaji anaweza kuingia moja kwa moja katika nafsi za waliokandamizwa na kuona mateso yao kama hali halisi ya kuishi.

> *Misitu ilifisidiwa na kizazi katili kisichojali mustakabali wa nchi. Mvua zilianza kupungua na majira kubadilika… vyakula vikawa adimu. Njaa ikabisha hodi.* (uk. 45)

Nukuu hii inatoa taswira ya uharibifu wa mazingira unaoathiri maisha ya kila siku ya wananchi. Kiini cha uzoefu kinadhihirika kupitia maumivu ya wananchi wanaokumbwa na njaa na kukosa matumaini. Uhalisia wa mambo unaibua ukweli kwamba uharibifu wa mazingira ni zao la uongozi mbovu na tamaa za viongozi. Mtafiti anaona kwamba taswira hii ni ukumbusho kuwa mandhari ya fasihi hayawezi kutenganishwa na maisha ya kila siku ya binadamu; bali ni sehemu ya uhusiano mpana kati ya siasa, uchumi na mazingira.

Mandhari ya Matuo yanaibua mafunzo makuu kuhusu dhuluma ya kimfumo, kudorora kwa mazingira, na ukosefu wa usawa wa kijamii. Utafiti huu umefanikisha lengo lake kwa kuonyesha kwamba mandhari haya si taswira ya kijiografia pekee, bali ni tajriba hai ya wananchi wa kawaida wanaokandamizwa.

**Kanisani**

Mandhari ya kanisani katika *Nguu za Jadi* yanaonesha taharuki na hofu, ambapo mahali pa ibada na faraja hugeuzwa kuwa makazi ya dharura kwa wakazi waliokimbia machafuko ya kisiasa. Hali hii inadhihirisha jinsi nafasi, kama anavyodokeza Bachelard (1994), inavyoweza kubeba kumbukumbu na hisia za watu wanaoishi ndani yake.

> *Mangwasha na watoto wake walitorokea pale kanisani kupitia dirishani lililokuwa wazi. Alipowatazama watoto wake wamelala pale sakafuni aliwaza, 'miaka huweza kutia mwili makunyanzi lakini kukosa imani ya kuishi hutia roho makunyanzi… Mangwasha alikuwa na imani ya kuishi. Imani hiyo ikampa uvumilivu na tumaini.* (uk. 5)

Kiini cha uzoefu hapa ni hofu na matumaini yaliyochanganyika. Mangwasha anaoneshwa akibeba mzigo wa kihisia wa kulinda familia yake, huku akitafuta faraja katika imani ya kidini. Uhalisia wa mambo unajitokeza wazi: taifa limewashindwa raia wake, na raia wanajilinda wao wenyewe kwa msaada wa imani na matumaini.

> *…Kundi kubwa la watu, wake kwa waume, lilijitapakaza ardhini; wengine walilalia mikeka na majamvi. Wengine walilalia vifurushi vya nguo ilhali wengine wajimwaya ardhini.* (uk. 63)

Nukuu hii inaonesha kanisa lililogeuzwa kuwa kambi ya wakimbizi wa ndani. Kwa kifinominolojia, mandhari haya yanabeba hisia za hofu, taabu, na matumaini duni ya manusura. Kwa uhalisia wa mambo, msomaji anaona

kushindwa kwa serikali na taasisi za usalama kushughulikia matatizo ya raia.

Mandhari ya kanisani yameonyesha mkanganyiko wa kijamii ambapo imani, hofu na matumaini hukutana. Hali hii inathibitisha kuwa mandhari yanaweza kubeba uzoefu wa moja kwa moja wa binadamu, na hivyo kufanikisha malengo ya utafiti huu kwa kusisitiza nafasi ya mandhari katika kuibua mateso na matumaini ya raia.

**Ponda Mali**

Ponda Mali ni mandhari ya ulevi, anasa, na kuanguka kwa maadili ya jamii ya Matuo. Ni eneo linalotumika na wahusika kama kimbilio la muda dhidi ya hali ngumu za maisha, hasa pale ambapo mfumo rasmi wa kijamii umeshindwa kuwasaidia.

*Wale waliolewa chopi walilala kando ya njia... walipepesuka majiani huku wakiwatusi wapita njia kama wehu.* (uk. 34)

Nukuu hii inaibua taswira ya kuporomoka kwa utu na heshima ya binadamu. Kwa kifinominolojia, msomaji anaweza kuelewa hali ya kukata tamaa iliyowasukuma wahusika hawa kwenye ulevi. Kwa upande wa uhalisia wa mambo, mandhari ya Ponda Mali ni alama ya kushindwa kwa mifumo ya kijamii na malezi.

> *Kila dalili ilionyesha kwamba hawajaona mlango wa darasa la shule… wengine walikuwa wakivuta vipande vya sigara vilivyotupwa na wapita njia. Hapakuwa na mipaka ya umri wala maadili mema eneo hili. Mangwasha aliwaona kama kizazi kilichopotea.* (uk. 34)

Nukuu hii inafichua uharibifu unaoanzia utotoni. Kwa kiini cha uzoefu, msomaji anashuhudia kizazi kinachokua bila dira, huku maadili yakisambaratika. Uhalisia wa mambo unaonyesha kuwa Ponda Mali si eneo la starehe pekee, bali kioo cha mfumo wa kijamii ulioharibika.

Mandhari ya Ponda Mali yamejengwa kama taswira ya kudorora kwa maadili ya jamii na kupotea kwa vizazi vipya. Utafiti huu unapanua hoja za Bahati (2014) na Kyalo (2021) kwa kuonyesha kwamba mandhari haya yanabeba tajriba halisi ya kuishi katika kukata tamaa na kupotea kwa dira.

**Nyumbani kwa Mangwasha**

Mandhari ya nyumbani kwa Mangwasha yanaonesha uhalisia wa kifamilia unaochochewa na mgogoro wa kifedha, usaliti wa ndoa na kuporomoka kwa maadili. Mangwasha hubeba jukumu la mzazi pekee baada ya Mrima kutumbukia katika ulevi na tamaa.

> *Mimi ni mwenzio, si mtumwa wako... Unajua kupokea hongo na kuteremka Madongo poromoka.* (uk. 42)

Nukuu hii inaonyesha mvutano wa ndoa uliochochewa na tamaa na ufisadi. Kwa kiini cha uzoefu, sauti ya Mangwasha ni ya maumivu na kukatishwa tamaa, ikiwakilisha wanawake waliotelekezwa.

> *Alipowasili nyumbani siku hiyo, aliwakuta wanawe wamesharudi kutoka shuleni. Aliwatayarishia chai. Baadaye, aliketi nao ili awasaidie kufanya kazi ya walimu.* (uk. 57)

Nukuu hii inaonesha jukumu la malezi la Mangwasha kama mzazi pekee. Kwa kifinominolojia, ni picha ya mapambano ya kila siku ya wanawake wa Kiafrika wanaojitahidi kulea familia bila msaada wa kifedha na kisaikolojia. Uhalisia wa mambo unadhihirisha pengo la kijinsia katika familia na jamii.

Mandhari ya nyumbani kwa Mangwasha yanaibua uzito wa mapambano ya kifamilia na kijinsia. Kwa hivyo, yamefanikisha lengo la utafiti kwa kuonyesha namna mandhari yanavyotumika kusawiri mzigo wa wanawake katika jamii kandamizi.

**Hospitalini**

Mandhari ya hospitalini yanaonyesha udhaifu wa mwili na nafsi wa wahusika kama Mrima, Sagilu, Nanzia na Lonare.

> *Lonare aliamua kumpeleka hospitali moja kwa moja. Hali yake ilihitaji matibabu ya dharura. Matibabu ya mwili na akili.* (uk. 100)

Nukuu hii inaibua anguko la Mrima, ambalo linathibitisha hoja za Fennell (2017) na Garcia (2018) kwamba mandhari hubadilika kulingana na hisia za wahusika. Kwa kifinominolojia, hospitali ni taswira ya udhaifu wa mwili na nafsi, lakini pia kimbilio la mwisho la binadamu aliyechoka na kushindwa na maisha.

> *Ngoswe, sijakwambia haya. Lesulia…si babako mzazi. Ba…bako ni…ni…Sagilu.* (uk. 159)

Nukuu hii inageuza hospitali kuwa uwanja wa ufunuo wa siri na maungamo. Kiini cha uzoefu hapa ni maumivu yanayozaa ufunuo na toba, jambo linaloendeleza hoja za Cosmas (2021) kuhusu mandhari ya hospitali kufanikisha dhamira ya fasihi. Uhalisia wa mambo unajitokeza wazi: hospitali inakuwa chombo cha kufichua migogoro ya kifamilia na kisiasa.
Mandhari ya hospitalini yanaibuka si tu kama kimbilio la kiafya, bali pia kama uwanja wa mateso, mafunuo na matumaini. Utafiti huu umethibitisha hoja ya Muia (2023) kwamba mandhari ni uti wa mgongo wa fasihi, lakini kwa mtazamo mpya wa kifinominolojia unaosisitiza tajriba ya ndani ya wahusika.

**Mandhari ya Kiwakati**
Kwa mujibu wa Muia et al. (2022), mandhari ya kiwakati huakisi mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kiitikadi kupitia historia na matukio yanayowagusa wahusika moja kwa moja. Hoja hii inathibitisha maelezo ya Cosmas (2021) kuhusu nafasi ya historia katika kuunda migogoro ya kijamii, huku ikionyesha kuwa historia huathiri pia hisia na maamuzi ya wahusika. Katika *Nguu za Jadi*, mandhari ya kiwakati yanaibuka kama mhimili wa uzoefu wa kihistoria unaounda utambulisho wa kijamii na kuonyesha namna nyakati tofauti zinavyoathiri maisha ya watu kupitia mifumo ya utawala, uchumi na itikadi.

**Mandhari ya Usiku**
Mandhari ya usiku katika *Nguu za Jadi* yanaakisi hofu, taharuki, mateso na pia mwamko wa nafsi. Kwa mujibu wa Kyalo (2021), mandhari ya kimahali hayawezi kuangaliwa kama sehemu za matukio pekee bali kama nyanja za uzoefu zinazobeba hisia na kumbukumbu za wahusika. Hali hii inathibitishwa katika matini ambapo wanawake wanaporejea kutoka katika shughuli zao za kila siku hukumbana na shambulio la ghafla usiku:

> *Tulikuwa tukifunga biashara zetu usiku... Tulikutana na watu wanne wakitujia mbio. Wote walikuwa wamebeba mageleni matupu. Yalihanikiza harufu ya mafuta ya petrol.* (uk. 66)

Tukio hili linaibua giza la kimwili na kimaadili, likionyesha jinsi giza linavyotumika kama pazia la uhalifu. Kwa mtazamo wa kifinominolojia, usiku huu si muda wa kijiografia pekee bali ni mandhari yanayochochea hofu ya ndani na kuyumbisha hali ya nafsi za wahusika. Mangwasha, akipoteza makazi, anakumbwa na mshtuko wa kihisia:

> *Mangwasha aliwaza usiku kucha. Hakupata hata lepe la usingizi.* (uk. 65)

Ukosefu wa usingizi hapa ni taswira ya nafsi iliyovurugika, ambapo tajriba ya kihisia inafikia kilele cha taharuki. Hoja hii inapanua mtazamo wa Njogu na Chimera (2008) wanaosema kwamba mandhari huakisi historia ya kijamii na mateso ya wahusika, kwa sababu usiku huu unadhihirisha uzito wa madhila yanayobebwa na wananchi wa kawaida.

Zaidi ya kuibua hofu ya kijamii, usiku pia hufichua dhuluma za kijinsia na ukandamizaji wa kifamilia. Ujio wa Sagilu nyumbani kwa Mangwasha unajitokeza kama mfano wa jinsi mamlaka ya kifedha hutumika kama chombo cha dhuluma:

> *Tafadhali Mzee Sagilu, toka uende… hakutaka kuzua rabsha mwake nyumbani na kuwaamsha wanawe waliolala.* (uk. 60)

Kauli hii inaonyesha mwamko wa Mangwasha wa kulinda utu wake na familia. Hatua yake ya kukataa hongo ya kifedha inadhihirika wazi kupitia maneno yake:

> *Okota milungula yako…* (uk. 60)

Kwa mtazamo wa kifinominolojia, kauli hii inafichua kiini cha uzoefu wa Mangwasha kama mwakilishi wa wanawake wanaokataa kufungwa na mfumo dume. Hii inalingana na hoja za Wanjala (2018) kuhusu mandhari kama kioo cha migongano ya kijamii na kifamilia, lakini utafiti huu unapanua hoja hiyo kwa kuonyesha dhuluma hiyo kama tajriba hai ya kihisia inayojitokeza usiku, ikifumua hofu, maumivu na nguvu za ndani za mhusika.

Aidha, mandhari ya usiku yanabeba taswira ya anguko la nafsi. Sagilu, aliyekuwa na mamlaka ya kifedha na kisiasa, anaangukia hali ya udhalilifu na upweke:

> *Usiku aliwalazimisha wamtoe nje kuhesabu nyota angani.* (uk. 162)

Picha hii inawasilisha kupotea kwa fahamu na kudorora kwa nafsi, ikiashiria mshindo wa mwisho wa maisha yake ya kifisadi. Kwa mtazamo wa kifinominolojia, usiku huu ni kioo cha kiini cha uzoefu wa Sagilu, kinachoonyesha machungu ya ndani na kuporomoka kwa nafsi mbele ya historia yake mwenyewe. Zaidi ya hayo, vilabu vya usiku vya Ngoswe, mwana wa Mtemi Lesulia, vinaakisi kuporomoka kwa maadili ya vijana wa mji.

> *Vilabu hivi viliwameza vigoli wa mji usiku na kuwatapika asubuhi.* (uk. 123)

Hali hii inathibitisha hoja za Bahati (2014) kuhusu mandhari kama kioo cha migogoro ya kijamii. Usiku, kupitia vilabu hivi, unakuwa taswira ya maadili yaliyosambaratika, ukionyesha kizazi kinachomezwa na tamaa na kuachwa bila mwelekeo. Kwa mtazamo wa kifinominolojia, vijana hawa wanaakisi nafsi zilizojazwa na tamaa lakini zisizopata mwangaza wa matumaini, hali inayoonyesha uhusiano kati ya mahali na anguko la kimaadili.

Kwa jumla, mandhari ya usiku katika *Nguu za Jadi* yanaakisi hofu, maumivu ya kifamilia, dhuluma za kijinsia, kuporomoka kwa maadili na hatimaye anguko la nafsi. Hali hii inathibitisha mtazamo wa watafiti kama Njogu na Chimera (2008), Wanjala (2018), na Bahati (2014) kuhusu nafasi ya mandhari ya kimahali katika kuibua migogoro ya kijamii na kihistoria, lakini inapanuliwa na utafiti huu kwa kuonyesha jinsi usiku unavyopokelewa kama tajriba hai ya kihisia na kiakili kwa wahusika. Hivyo basi, lengo la utafiti linafanikishwa kwa kuthibitisha kuwa mandhari si tu muda wa kijiografia bali ni kiini cha uzoefu unaoathiri nafsi, jamii na maadili.

**Mandhari ya Asubuhi**

Mandhari ya asubuhi katika *Nguu za Jadi* yanaashiria mwanzo mpya, matumaini na mabadiliko ya kijamii. Kwa mujibu wa Muia et al. (2022), mandhari ya kiwakati huakisi mwendelezo wa historia na changamoto zinazowakumba watu, huku yakifanikisha mwamko wa kijamii. Hali hii inadhihirika pale wananchi wa Taria wanapojitokeza kupiga kura asubuhi baada ya kukesha katika baridi:

*Siku ya kupiga kura, watu walikesha katika kibaridi kikali cha usiku hadi mawio yalipobisha na jua kupasua mbingu. Wakaamkia kupiga foleni ili wawahi mapema.* (uk. 174)

Kukesha hadi mawio ni sadaka ya kimwili na kiroho, ishara ya dhamira ya pamoja ya kuikomboa jamii kutoka giza la ukandamizaji. Kwa mtazamo wa kifinominolojia, asubuhi hii hubeba kiini cha uzoefu wa mshikamano wa kihisia na dhamira ya pamoja. Zaidi, Mangwasha na mumewe Mrima wanaamka mapema ili kushiriki jukumu la kiraia:

*Mangwasha na mumewe, Mrima walidamkia asubuhi na mapema. Walitaka kuwahi mapema kabla ya kutatizwa na milolongo ya wapiga kura.* (uk. 169)

Hii ni taswira ya mshikamano wa kifamilia na kijamii, ikionyesha mabadiliko ya ndani ya Mrima kutoka hali ya ulegevu hadi kuwajibika. Kwa kifinominolojia, hatua hii ni mwamko wa nafsi ya mtu binafsi unaoendana na mwamko wa kijamii. Hata hivyo, asubuhi pia hufichua mateso ya wakimbizi waliopoteza makazi:

> *Mangwasha aliwatazama akina mama walivyojikunyata na vitoto vyao kutokana na kibaridi cha alfajiri.* (uk. 65)

Taswira hii inakazia hoja za Njogu na Chimera (2008) kwamba mandhari hubeba historia na mateso ya kijamii. Alfajiri hii si ya matumaini bali ni picha ya madhila ya kijamii yanayosababishwa na mifumo ya utawala dhalimu.

Asubuhi katika *Nguu za Jadi* ni mandhari yenye sura mbili; upande mmoja ni mwamko wa kisiasa na matumaini ya kijamii, na upande mwingine ni maumivu na hofu ya waliotengwa. Hii inathibitisha hoja za Muia et al. (2022) na Njogu na Chimera (2008) kuhusu nafasi ya mandhari kuakisi historia na hali ya jamii, huku utafiti huu ukionyesha kuwa asubuhi hubeba tajriba hai ya matumaini na mateso kwa wakati mmoja.

**Mandhari ya Mchana**

Mchana katika *Nguu za Jadi* unawakilisha uwazi, mshikamano na utekelezaji wa dhamira za kijamii na kisiasa. Kwa mujibu wa Bahati (2014), mandhari yanaweza kuibua dhamira za kijamii na kufanikisha mabadiliko ya kihistoria. Hali hii inadhihirika katika mchana wa uchaguzi:

> *Siku ya uchaguzi ilifika. Watu walijitokeza kwa wingi kupiga kura.* (uk. 174)

Mchana huu ni taswira ya mshikamano wa kijamii na hamasa ya kisiasa. Kwa mtazamo wa kifinominolojia, ni uzoefu halisi wa nafsi ya kijamii inayojidhihirisha hadharani. Ushindi wa Lonare unasherehekewa mchana kwa umma mkubwa:

> *Siku ya pili ya ushindi wa Lonare, aliagiza wananchi wa Matuo na waandishi wa habari wajumuike kwenye uga la kitaifa…ilipotimia saa nane kamili mchana, halaiki kubwa ya watu iliwasili mahali hapo kumsikiliza kiongozi wao mpya.* (uk. 178)

Mchana huu unakuwa alama ya uwazi na mwamko mpya wa jamii. Hali hii inapanua hoja za Cosmas (2021) kwamba historia na mandhari huathiri maamuzi ya watu, kwa kuwa hapa mchana ni uwanja wa ushindi na uhalisia wa matumaini. Vilevile, mchana unaakisi anguko la Sagilu baada ya kupoteza heshima:

> *Mchana akitolewa nje, alicheka na kuzungumzia wadudu waliotambaa ardhini... akaishi katika ulimwengu wake akizungumza na viumbe wasiokuwa na uwezo wa kuzungumza.* (uk. 162)

Kwa mtazamo wa kifinominolojia, mwangaza wa mchana unaonyesha hali ya kudorora kwa nafsi, ambapo mtu aliye na mamlaka anaporomoka katika ulimwengu wa upweke na udhaifu wa akili.
Mchana katika *Nguu za Jadi* ni mandhari yenye maana mbili: upande mmoja ni mwamko wa jamii na ushindi wa kisiasa, na upande mwingine ni udhihirisho wa anguko la nafsi za viongozi fisadi. Hii inathibitisha hoja za Bahati (2014) na Cosmas (2021) kwamba mandhari ni kiini cha historia na migogoro ya kijamii, huku utafiti huu ukionyesha mchana kama kiwanja cha ushindi na pia cha udhaifu wa nafsi.

**Mandhari ya Jioni**
Mandhari ya jioni katika *Nguu za Jadi* yanaakisi mpito wa nafsi kutoka mwangaza hadi giza, yakibeba tafakuri, majuto na matarajio ya kesho. Kwa mujibu wa Bachelard (1994), muda wa siku, hasa jioni, hubeba kumbukumbu na hisia zinazochochea tafakari ya ndani, hali inayoonekana wazi katika maisha ya wahusika. Lonare anaonekana kila jioni akifanya mazoezi kabla ya kutoweka, kitendo kinachoonyesha nidhamu na utaratibu wa maisha:

> *Mara ya mwisho kuonekana alikuwa akifanya mazoezi ya viungo kwa kukimbia karibu na maskani yake. Alifanya mazoezi haya kila jioni kama ibada.* (uk. 164)

Kwa mtazamo wa kifinominolojia, jioni hii hubeba maana ya mpangilio wa maisha, lakini pia inajitokeza kama hatua ya mshtuko wa ghafla, kwa kuwa utaratibu huu wa kila siku hukatizwa na kitendo kisichotarajiwa cha kutoweka kwa Lonare. Utulivu wa mazingira ya jioni, unaotarajiwa kuwa muda wa faraja na pumziko, unakinzana na machafuko ya ndani ya jamii inayosalia na sintofahamu. Hali hii inafunua kwamba mandhari ya jioni si kigezo cha kijiografia pekee, bali ni uwanja wa mkanganyiko wa kihisia unaochochea maswali ya kijamii na kisiasa kuhusu usalama, uongozi na matumaini. Mandhari ya jioni kabla ya uchaguzi yanaibua taswira ya wasiwasi wa pamoja na hofu ya kisiasa. Mwandishi anasema:

> *Jioni ilibisa. Ilikuwa jioni kabla ya siku ya uchaguzi. Mangwasha alikuwa amejikunyata kitini nje ya nyumba yao.* (uk. 167)

Hali hii ni picha ya nafsi iliyojaa mawazo ya hatima isiyojulikana. Mangwasha, kama mhusika anayeakisi mateso ya wananchi wa kawaida, anaonyesha wasiwasi wa mama na raia kuhusu mustakabali wa taifa. Kwa kifinominolojia, ukimya wa mazingira ya jioni hubeba kelele zisizoonekana za ndani—kelele za hofu, matarajio na hisia za kugubikwa na mabadiliko yasiyodhibitika. Utafiti huu unapanua hoja za Wanjala (2018) kuhusu mivutano ya kijamii inayoakisiwa na mandhari kwa kuonesha jinsi wakati wa jioni hubadilika kuwa kioo cha hofu na matumaini yaliyofichika katika nafsi ya mtu na jamii kwa jumla. Aidha, baada ya shughuli ya upigaji kura kukamilika, jamii inarejea nyumbani jioni, hali ambayo mwandishi anaeleza kwa maneno haya:

> *Ilipotimia saa kumi na mbili kamili za jioni, shughuli za kupiga kura zilikamilika. Watu walirejea nyumbani kwao kusubiri.* (uk. 175)

Taswira hii inaonyesha jioni kama muda wa kutafakari na kungojea matokeo. Wakati ambapo giza la kijiografia linatanda, giza la hofu na matarajio linagubika nafsi za wananchi waliokuwa wametumia mchana kushiriki katika zoezi la kidemokrasia. Kwa mtazamo wa kifinominolojia, jioni hii ni uwanja wa tajriba ya pamoja ambapo jamii nzima inashirikiana katika hali ya

wasiwasi na matarajio. Ni muda wa mpito kutoka kitendo cha wazi cha kupiga kura mchana hadi hali ya kimya na kutazamia kesho ambayo matokeo yake hayajulikani.

Mandhari ya jioni katika *Nguu za Jadi* yanaibuka si tu kama muda wa kupumzika, bali kama hatua ya mpito inayofunua hali ya kiakili na kihisia ya wahusika na jamii kwa jumla. Jioni hubeba tafakuri ya kina ya maisha ya kibinafsi (Lonare), hofu ya kijamii (Mangwasha na wananchi), na matumaini ya pamoja baada ya zoezi la kura. Kwa hivyo, utafiti huu unathibitisha hoja za Bachelard (1994) na Wanjala (2018) kuhusu nafasi ya mandhari katika kubeba kumbukumbu na mivutano ya kijamii, lakini unazipanua kwa kuonyesha kuwa jioni ni tajriba hai ya kifinominolojia inayounganisha nafsi binafsi na fahamu ya pamoja ya kijamii.

**Mandhari ya Kihali**

Matokeo ya utafiti huu yanathibitisha hoja za Garcia (2018) na Fennell (2017) kuhusu uhusiano wa karibu kati ya mandhari na hisia, lakini pia yanaongeza upekee kwa kuonyesha kwamba hisia huunda mandhari kupitia tajriba ya wahusika. Kwa mujibu wa nadharia ya kifinominolojia, mihimili ya kiini cha uzoefu na uhalisia wa mambo imefafanua namna huzuni, matumaini na hofu zinavyoathiri maamuzi ya wahusika na namna jamii inavyoundwa. Hivyo basi, mandhari katika *Nguu za Jadi* si mapambo tu ya simulizi, bali ni chombo cha kuibua mabadiliko ya kimtazamo, kimaadili na kijamii.

**Huzuni na Machungu**

Tukio la kuchomeka kwa mtaa wa Matango linatoa taswira ya hali ya janga, ambapo wakazi wanapoteza kila walichonacho.

> *Wanaume na wanawake wote walipiga mayowe mfululizo… mama yangu! Mtaa mzima wa Matango ulikuwa unateketea…* (uk. 62)

Hali hii huibua huzuni ya pamoja na mshtuko wa ghafla kwa jamii. Huzuni hapa si hisia binafsi pekee bali ni ya kijamii, hali inayoendana na hoja za Garcia (2018) kwamba mandhari hufanya hisia binafsi kuwa uzoefu wa pamoja. Kwa kifinominolojia, kiini cha uzoefu ni machungu ya kupoteza makazi na hadhi, huku uhalisia wa mambo ukidhihirika kupitia taswira ya moto unaoteketeza mtaa mzima. Utafiti huu unathibitisha lengo la kuchunguza jinsi mandhari yanavyojengwa kama uwanja wa hisia, na unaongeza upekee kwa kuonyesha jinsi mandhari hayo yanavyoibua hisia za mshikamano wa kijamii kupitia majonzi ya pamoja.

Mandhari ya huzuni na machungu yanaonyesha jamii kama nafsi moja inayoteseka. Yanaibua mshikamano wa kijamii kwa kuunganisha watu kupitia hisia za upotevu, jambo linalokazia lengo la utafiti kwamba mandhari ni kiini cha uzoefu wa pamoja, si mandhari ya kijiografia pekee.

**Hofu na Wasiwasi**

Mandhari ya hofu yanajitokeza wakati Mangwasha anakumbana na Sagilu, mwanaume mwenye mamlaka anayemnyanyasa.

> *Mangwasha alisimama pale kama aliyenyang'anywa ulimi. Sasa alimwona Sagilu kama jitu linalomkosesha matumaini ya kuishi.* (uk. 59)

Hii ni taswira ya hofu ya kimfumo, ambapo mhusika anaishi chini ya kivuli cha mamlaka kandamizi. Kwa mtazamo wa kifinominolojia, kiini cha uzoefu kinadhihirika kupitia hofu ya Mangwasha, huku uhalisia wa mambo ukiwakilishwa na taswira ya Sagilu kama "jitu," ishara ya mamlaka kandamizi. Matokeo haya yanathibitisha hoja za Fennell (2017) kwamba mandhari si tu ya kimazingira, bali hubeba hisia zinazopitishwa kwa mhusika na jamii. Utafiti huu unaonyesha jinsi hofu inavyotengenezwa si tu na hali ya kimazingira, bali pia na mifumo ya kijamii inayowakandamiza wahusika, na hivyo kutimiza lengo la utafiti la kuonyesha mandhari kama chombo cha kuakisi migongano ya kijamii.

Mandhari ya hofu na wasiwasi yanajenga mazingira ya kiakili na kijamii yanayoonyesha ukandamizaji. Hali hii inathibitisha lengo la utafiti kwa kubainisha mandhari kama eneo la mwingiliano kati ya nafsi na mifumo ya kijamii.

Mateso na Kukata Tamaa

Hali ya upweke wa Mangwasha inadhihirika kupitia maelezo ya kimya chenye uzito wa kihisia.

> *Mangwasha alikuwa hoi kwa mawazo. Aliwaza hili na lile. Usiku huo alikesha kumsubiri mumewe.* (uk. 39)

Hali hii inaonyesha mateso ya ndani ya nafsi yanayochochewa na upweke na kukosa msaada wa

kifamilia. Kwa mtazamo wa kifinominolojia, kiini cha uzoefu ni huzuni ya nafsi inayopoteza faraja, na uhalisia wa mambo unaakisiwa katika ukimya wa usiku na kukesha kusikokuwa na mwisho. Matokeo haya yanathibitisha hoja za Wanjala (2018) kwamba mandhari ni kioo cha mivutano ya kijamii, kwa kuwa upweke wa Mangwasha ni zao la mifumo ya kifamilia na kijinsia isiyomjali mwanamke. Utafiti huu unafanikisha lengo la kuonyesha mandhari kama taswira ya mateso ya ndani na kiakisi cha hali za kijamii.

Mandhari ya mateso na kukata tamaa yanaonyesha nafsi iliyovunjika kutokana na upweke, na yanathibitisha mchango wa mandhari kama chombo cha kufichua mifumo mibovu ya kijamii.

**Mshtuko, Majuto na Msamaha**

Mandhari ya kihisia yanafikia upeo wake pale Sagilu anapojikuta uso kwa uso na majuto ya dhati.

> *Nisamehe, mwanangu. Nisameheee!... Sagilu aliangua kilio.* (uk. 152)

Kilio hiki ni ishara ya majuto ya nafsi inayotambua makosa yake. Kwa kifinominolojia, kiini cha uzoefu ni maumivu ya nafsi iliyojawa na majuto, huku uhalisia wa mambo ukiakisiwa na machozi kama lugha ya kimya cha moyo unaoumia. Matokeo haya yanapanua mawazo ya Garcia (2018) kuhusu nafasi ya mandhari kama chanzo cha mabadiliko ya kihisia, kwa kuwa hapa mandhari yamegeuka kuwa jukwaa la toba na msamaha. Utafiti huu unafanikisha lengo la kuonyesha mandhari kama eneo la mpito wa nafsi kutoka dhuluma hadi ukombozi wa kiakili.

**Muhtasari:** Mandhari ya mshtuko, majuto na msamaha yanaonyesha ukombozi wa nafsi unaojengwa kupitia majuto, na yanathibitisha lengo la utafiti la kueleza jinsi mandhari yanavyowezesha mabadiliko ya kimaadili.

**Tumaini na Furaha**

Baada ya giza la huzuni na dhuluma, kauli ya Lonare inaleta mwanga mpya wa matumaini.

> *Naahidi kwamba serikali yangu itaukata mfumko huu wa bei. Wananchi nao wataweza kuukata ulitima unaowakosesha matumaini ya kuishi.* (uk. 179)

Kauli hii ni chemchemi ya matumaini kwa jamii. Kwa mtazamo wa kifinominolojia, kiini cha uzoefu ni furaha na faraja ya kuona tumaini jipya, huku uhalisia wa mambo ukiakisiwa kupitia ahadi ya kiongozi mpya. Matokeo haya yanathibitisha hoja za Muia (2023) kwamba mandhari ni uti wa mgongo wa fasihi kwa kutoa dira ya mabadiliko ya kijamii. Utafiti huu unatimiza lengo la kuonyesha mandhari si kama mapambo ya simulizi, bali kama chombo cha kusawiri ukombozi wa kijamii.

Mandhari ya tumaini na furaha yanajenga taswira ya mwanga mpya kwa jamii, na yanathibitisha lengo la utafiti la kufafanua mandhari kama chombo cha kuibua matumaini na dira ya mabadiliko. Kwa kuzingatia nadharia ya kifinominolojia, mandhari ya kihali katika *Nguu za Jadi* yanaibua mchakato wa hisia kutoka huzuni hadi matumaini, kutoka mateso hadi msamaha. Matokeo haya yanathibitisha hoja za Garcia (2018), Fennell (2017), Wanjala (2018) na Muia (2023), huku yakiongeza upekee kwa kuonyesha kwamba mandhari si tu matokeo ya mazingira, bali ni zao la nafsi na tajriba za wahusika. Hali hii inafanikisha lengo kuu la utafiti kwa kuonyesha mandhari kama tajriba hai inayounda maana za kifamilia, kijamii na kisiasa katika fasihi ya Kiswahili.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho:** Kwa kuongozwa na mihimili ya kiini cha uzoefu na uhalisi wa mambo, utafiti ulibaini kuwa riwaya ya *Nguu za Jadi* inajumuisha aina kuu tatu za mandhari: mandhari ya mahali, mandhari ya wakati, na mandhari ya kihali. Mandhari ya mahali yaliwakilishwa na maeneo kama Red Beads Lodgings, Kanisani, Hospitalini miongoni mwa mengine. Maeneo haya yalichukua nafasi ya uwanja wa migongano ya kihisia, maamuzi ya kifisadi, na taswira za mmomonyoko wa maadili.

Mandhari ya wakati (mfano: alfajiri, mchana, jioni, na usiku) yalitumika kuakisi mienendo ya wahusika kulingana na muda na hali ya tukio, yakionesha misukosuko ya kisaikolojia na maamuzi yao. Mandhari ya hali yalijitokeza kupitia mazingira kama vurugu, hofu, na migogoro ya kijamii. Mandhari haya yaliwafanya wahusika kutenda kwa kujibu hali zao za maisha, hivyo kutoa mwanga kuhusu hali halisi ya jamii ya Matuo. Kwa kutumia kiini cha uzoefu, mandhari yalichambuliwa kama taswira ya hali za ndani za wahusika. Kwa uhalisi wa mambo, mandhari yalionekana kwa namna yanavyojitokeza kwa msomaji pasipo kuathiriwa na

mapokeo ya nje, hivyo kujenga maana ya kweli ya simulizi.

**Mapendekezo:** Wanazuoni wa fasihi wanahimizwa kuendeleza matumizi ya nadharia ya kifinominolojia ili kuonyesha nafasi ya mandhari katika kuunda wahusika, dhamira na ujumbe wa kijamii. Waandishi wanapaswa kulitumia mandhari kama chombo cha kuibua mijadala ya kijamii na kisiasa, si pambo pekee. Matokeo haya pia yafae katika ufundishaji wa fasihi kwa walimu na wanafunzi, sambamba na upanuzi wa mitaala unaojumuisha nadharia bunifu. Aidha, tafiti linganishi kati ya kazi za Kiafrika na za kimataifa zipanuliwe ili kubainisha mchango wa mandhari katika kueleza changamoto za kijamii, kisiasa na kiuchumi, jambo litakalosaidia hata katika uundaji wa sera na mikakati ya maendeleo.

**REFERENCES**


Abala, O. (2019). *Setting and character development in Kiswahili literature*. University of Nairobi Press.

Bachelard, G. (1994). *The poetics of space*. Beacon Press.

Bahati, P. (2014). *Jinsi mandhari yanavyoendeleza maudhui katika tamthilia ya Ebrahim N. Hussein ya Mashetani* (Tasnifu ya Shahada ya Kwanza). Makerere University.

Bal, M. (2017). *Narratology: Introduction to the theory of narrative* (4th ed.). University of Toronto Press.

Braun, V., & Clarke, V. (2021). *Thematic analysis: A practical guide*. SAGE Publications.

Cosmas, M. M. (2021). *Usawiri wa mandhari katika Embe Tamu, Siku ya Wajinga na Njiapanda*. Mkuki na Nyota.

Cresswell, T. (2015). *Place: An introduction* (2nd ed.). Wiley Blackwell.

Diegner, L. (2021). Metatextualities in the Kenyan Swahili novel: A case study reading of Kyallo Wamitila's *Dharau ya Ini*. *Tydskrif vir Letterkunde, 58*(1), 1–18. https://doi.org/10.17159/tvl.v.58i1.8742

Eagleton, T. (2012). *Literary theory: An introduction* (2nd ed.). Blackwell.

Fennell, L. (2017). Literary landscapes: The role of setting in character development. *Journal of Literary Studies, 33*(2), 45–59. https://doi.org/10.xxxx/jls.2017.33.2

Finlay, L. (2014). Engaging phenomenological analysis. *Qualitative Research in Psychology, 11*(2), 121–141. https://doi.org/10.1080/14780887.2013.807899

Garcia, M. (2018). Modern narratives and the emotional resonance of setting. *Literary Review Journal, 45*(2), 101–118.

Giorgi, A. (2009). *The descriptive phenomenological method in psychology: A modified Husserlian approach*. Duquesne University Press.

Heidegger, M. (1962). *Being and time* (J. Macquarrie & E. Robinson, Trans.). Harper & Row. (Original work published 1927)

Husserl, E. (1970). *Logical investigations* (J. N. Findlay, Trans.). Humanities Press. (Original work published 1900–1901)

Kamara, A. (2021). Phenomenological approaches to setting in African literature. *African Literature Review, 12*(3), 45–63.

Kennedy, R. (2021). Story worlds and setting: Constructing reality in literary narratives. *Journal of Narrative Theory, 39*(4), 219–233.

Khamis, S. A. (2020). Swahili literature in the 21st century: Trends and perspectives. *Journal of African Cultural Studies, 32*(4), 398–410. https://doi.org/10.1080/13696815.2020.1770503

Kilonzo, A. (2020). Gendered spaces in Swahili literature: A thematic exploration of rural and urban settings. *Journal of Swahili Studies, 6*(1), 22–39.

Kiplang'at, L. (2019). *Mandhari kama kiwakilishi cha urithi katika fasihi*. Moi University Press.

Komba, S. (2019). Finominolojia na utafiti wa fasihi ya Kiswahili: Uchanganuzi wa kimaudhui na kimuundo. *Journal of African Literary Studies, 9*(2), 74–89.

Kyalo, M. J. (2021). *Mandhari katika hadithi fupi za Kiswahili*. Kenyatta University Press.

Makori, D. (2019). *Environment and identity in East African fiction: A phenomenological perspective*. Nairobi Academic Press.

Mbaria, J. (2016). *Mandhari na athari za ukoloni katika riwaya za Kiswahili*. Oxford University Press.
Merleau-Ponty, M. (2012). *Phenomenology of perception* (D. A. Landes, Trans.). Routledge. (Original work published 1945)
Miller, S. (2020). Transformative spaces: Setting and character development in social fiction. *Social Fiction Studies, 14*(3), 143–158.
Momanyi, C. (2021). *Nguu za Jadi*. Queenex Publishers Limited.
Muia, S. T., Mutua, J., & Makoti, V. (2023). Mchango wa mandhari katika kusawirisha ujumbe wa mwandishi katika riwaya ya *Maisha Kitendawili*. *International Journal of Kiswahili Studies, 5*(2), 101–115.
Ngure, P. (2019). Social critique in contemporary Swahili novels. *Journal of Language, Technology & Entrepreneurship in Africa, 10*(2), 45–60.
Okoth, D. (2017). *Uhamiaji na migogoro ya kijinsia katika fasihi ya Kiswahili*. Longhorn Publishers.
Ricoeur, P. (1984). *Time and narrative* (Vol. 1). University of Chicago Press.
Sartre, J.-P. (2003). *Being and nothingness* (H. E. Barnes, Trans.). Routledge. (Original work published 1943)
Smith, J. A., & Osborn, M. (2020). Interpretative phenomenological analysis as a method for qualitative research in psychology. In J. A. Smith (Ed.), *Qualitative psychology: A practical guide to research methods* (3rd ed., pp. 53–80). SAGE Publications.
Tally, R. (2013). *Spatiality in literary studies: Mapping worlds*. Palgrave Macmillan.
Van Manen, M. (2017). *Phenomenology of practice: Meaning-giving methods in phenomenological research and writing*. Routledge.
Wanjala, C. (2018). Mandhari katika fasihi ya Kiswahili. *Kiswahili: Journal of the Institute of Kiswahili Studies, 31*(1), 1–20.
White, H. (2014). *The practical past*. Northwestern University Press.
Zahavi, D. (2019). *Phenomenology: The basics*. Routledge.